TANGAZO LA SERIKALI Na. 676 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA SEKONDARI YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Sekondari ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

*Tangazo La Serikali Na. 676 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye njia panda kati ya barabara za Mlowa na Manyerere kwenye alama yenye majira - nukta 703081E, 9021225N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa kufuata barabara ya Mlowa kwa umbali wa kilomita 2.603 hadi alama yenye majira – nukta 705199E, 9019766N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara inayoelekea Shule ya Sekondari ya Maguvani na mkondo wa maji ya mvua ya Igangidungu kwa umbali wa kilomita 1.664 hadi kwenye alama yenye majira - nukta 704231E, 9018521N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata mkondo wa maji ya mvua ya Igangidungu kwa umbali wa kilomita 2.397 hadi mahali ambapo mkondo wa maji ya mvua unakutana na barabara ya Manyerere kwenye alama yenye majira - nukta 702589E, 9020342N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini hadi barabara ya Manyerere kwa umbali wa kilomita 1.021 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*